# Pambazuko

Toleo Namba 0044 Jumatatu Agosti 28-Septemba 3, 2023


# Brics sasa yatamani Tanzania

● *Chanzo: Utajiri wa rasilimali, eneo mkakati, amani*



*Rais Samia Suluhu Hassan*

*Uk. 9, 10&11*



*Waziri Mkuu wa India Narendra Modi*



*Rais wa Russia Vladimir Putin*



*Rais wa Brazil Luiz Lula da Silva*



*Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa*

# Usinywe sumu kuua adui - Bagonza

**Uk. 4**

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

# Tahariri

## Kila mmoja asaidie kutokomeza

TANZANIA ni miongoni mwa nchi tano za Afrika ambazo zinatajwa kuwa zitakuwa zimetokomeza maambukizi mapya ugonjwa wa Ukimwi ifikapo mwaka 2023.

Hakika taarifa hii imejaa matumaini makubwa kwani sasa vifo na maambukizi ya magonjwa mengine nyemelezi yaliyokuwa yakikomazwa na kusambaa kwa Ukimwi (HIV), yatakoma.

Umoja wa Mataifa umetangaza kwamba dunia iko mbioni kutokomeza Ukimwi ifikapo mwaka 2030, lakini hatua hii itafanikiwa zaidi endapo programu muhimu za afya zitakapofadhiliwa kikamilifu.

Inaelezwa na Umoja wa Mataifa (UN) kuwa eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara – Bara la Afrika, ambako asilimia 65 ya watu wote wenye maambukizi ya Ukimwi wanaishi, litakuwa huru na kuondokana na hofu ya maambukizi mapya.

Tanzania inatajwa kufikia lengo ushindi wa mapambano dhidi ya Ukimwi kwa uwiano wa '95-95-95.'

Umoja wa Mataifa kupitia shirika lake la kupambana na Ukimwi, UNAIDS, unabainisha kwamba asilimia 95 ya watu wanaoishi na ugonjwa huo wanajua hali zao, asilimia 95 ya watu wanaojua hali zao wanatumia dawa kurefusha maisha, na asilimia nyingine 95 ya watu wanaopata matibabu wamevifubaza virusi vinavyoambukiza ugonjwa huo uliotikisha dunia kwa miongo mingi.

Mkurugenzi Mtendaji wa UNAIDS, Winnie Byanyima anaeleza kufurahia hatua hiyo kama ambavyo dunia imepokea kwa furaha hatua hiyo.

Hata hivyo, hatua hiyo haitakuwa na maana ikiwa kila nchi, ikiwamo Tanzania itabweteka na kukaa kusubiri misaada kutoka UN ili kuukabili na hatimaye kuutokomeza ugonjwa huo.

Jitihada za Tanzania – kupitia wizara yake ya afya, kuukabili ugonjwa huo, zimekuwa zikisifika kwa kutoa taarifa sahihi, kusambaza dawa na kuhimiza kutumika kwa wakati; na kupewa kwa wahusika sahihi, kutunza kumbukumbu na kutangaza njia za kujikinga mara kwa mara.

Mara kadhaa UNAIDS imesifia jitihada za Tanzania kupambana na Ukimwi na imekuwa ikipigiwa mfano kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika.

Hata hivyo, pamoja na habari hizo njema na Tanzania kuwa kinara wa kutokomeza maambukizi ya Ukimwi, bado sisi katika Pambazuko tunaamini kuwa juhudi za mtu mmoja mmoja, zinahitajika zaidi ili kuhakikisha Ukimwi unatokomezwa hata kabla ya kufikia 2030.

Ikiwa kila Mtanzania atajikita kulinda afya yake na ile ya wengine, uhakika ni kwamba Ukimwi hautakuwa janga tena kutisha hatma ya uhai wa taifa letu.

Pambazuko tunaendelea kuhimiza watu kupima kujua afya zao na kujiepusha na ngono, ikiwa kuna ulazima wa kufanya ngono, basi wahusika wahakikishe wanazingatia matumizi sahihi ya kinga.

Tunaamini kuwa mwisho wa kusambaa kwa ugonjwa wa Ukimwi ni fursa ya urithi wenye nguvu ya kipekee kwa ustawi wa Tanzania na watu wake.

Inawezekana, kila mtu atende wajibu wake.

# HONGERA BINTI...................



*Mkurugenzi wa Bodi ya Shule ya Mwalimu JK Nyerere, Salva Rweyemamu, akikabidhi cheti kwa Rahma Mboweto, mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo wakati wa sherehe za mahafali yake ya 25 juzi – Jumamosi. Shughuli hiyo ilifanyika katika viwanja vya shule hiyo, Mbezi Beach jijini Dar es Salaam. Kulia mjumbe wa bodi ya shule hiyo, Kodi Ralph Siara. (Picha na Mpigapicha Maalum).*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## NUKUU



***Ni vyema na haki kwa kila mmoja wetu kukumbuka kujivua mzigo wa kiburi cha cheo au mali, na ajitwishe hisani, ubinadamu na tafakuri ya kujiweka katika viatu vya mwenzake. Hakika kiburi siyo maungwana na dhamana na mali huisha, lakini utu hudumu na kukumbukwa kwa mema daima - Abdulsamad Abdulrahim (mbobezi katika sekta ya nishati na madini Tanzania).***

## Tafakuri

# Usinywe sumu kuua adui yako - Bagonza

KUNA hisia kwamba katika uchaguzi wa kumpata mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Tanzania (KKKT) uliofanyika Alhamisi iliyopita – Agosti 24, Arusha; haukuwa wa haki.

Zipo dalili nyingi, lakini kubwa ni kuondoshwa kwa baadhi ya waliokuwa wakitarajiwa kugombea na hata kupewa nafasi kubwa - ya mmoja wao kuibuka mshindi.

Nyingine ni kuwepo kwa kura zilizoharibika. Hii haiingii akilini kwa "watu wa Mungu" – tena wakiwa wasomi wa upeo katika masuala ya demokrasia, imani na hata utaua; kwa maana ya kutenda yale yaliyo mema na haki.

Mara nyingi, kura uharibika kwa watu wasiokuwa na weledi na wengine wenye "utukutu" wa kuamua kuharibu kura, lakini kwa wasomi hubeba tafsiri nyingi tofauti. Moja ya tafsiri hizo ni kwenda kinyume na wote waliopitishwa ama "kususia uchaguzi."

Mmoja wa maaskofu waliokuwa wakipewa nafasi ya kuingia kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi huo ni Askofu Dkt. Benson Bagonza, Mkuu wa KKKT - Dayosisi ya Karagwe.

Ambaye ameamua kuandia waraka huu wenye kutafakarisha;

Wapendwa, nimejizuia sana kuandika au kusema chochote, lakini mmenisonga sana, mkitaka niseme neno. Nipo safarini kuelekea Vienna, Austria. Na kwa kuwa sijui kama nitafika niendako kabla hamjakata tamaa ya kunisikiliza, basi naomba niseme mambo haya matatu na myasome kwa furaha.

Kwanza; tumetazamwa na dunia nzima kwa siku nne (tukiwa kwenye mkutano mkuu wa KKKT pale Arusha). Mtu mmoja ambaye ni mara ya kwanza kushiriki mkutano huo, alipoona yaliyotokea aliniuliza; "Hivi nyie wenzetu Wachungaji na Maaskofu mmeshagundua kwamba mbingu haipo mkafanya iwe siri yenu tu?" Akaongeza, "kama mbingu ipo kwanini mfanyiane mabaya hivi? Tena hadharani?"



*Askofu Dkt. Benson Bagonza*

Pili; nilizoeshwa kuamini kuwa watu wanakataliwa kwa sababu ya ubaya wao na wengine hupendwa kwa sababu ya wema wao, lakini sasa nimeamini wapo wanaoweza kukataliwa kwa sababu ya wema wao na wengine wakapendwa kwa sababu ya ubaya wao.

Kikubwa nilichojifunza ni kuwa ubaya hauwezi kukaa kwa amani na wema.

Tumefundishwa, katika Agano la Kale, kwamba kichafu kikigusana na kitakatifu, kile kitakatifu kinaharibika (kunajisika). Lakini katika Katika Agano Jipya, kichafu kikigusana na kitakatifu, kile kichafu kinatakasika. Je KKKT ni ya Agano Jipya au la Kale?

Tatu; watu wakatili na waovu hujiandaa kupiga na kuangamiza wabaya wao wakati wote. Watu wema hutafuta kuushinda ubaya kwa wema wakati wote. Kuna wakati wapigaji wakishapiga, huketi na kufurahi kuwa wamepiga, hata hivyo, wakitulia hugundua kuwa kumbe wao ndio wamepigwa sana.

Nimesamehe yote. Kutosamehe ni sawa na kunywa sumu ukitegemea afe adui yako. Sumu uliyokunywa bila kukusudia inaua vibaya kuliko uliyokunywa kwa kukusudia.

Huku kwetu (KKKT) huwa hatugombei, bali tunagombezwa na kuzodolewa. Amani ya Kristo iwe nawe.

# Askofu Munga amuasa Bagonza

**Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA**

AWALI ya yote nawapongeza Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kwa kumaliza Mkutano Mkuu kwa utulivu.

Sitaki kuingilia mipango na makusudi ya Mungu. Lakini naandika hapa ikiwa ni kama maombolezo kwani nilijua kuwa ungefanyiwa dhuluma na vitimbwi vya wazi mchana kweupe, ili jina lako lisiteuliwe na kupelekwa mbele kwa ajili ya kupigiwa kura na wajumbe wa sinodi ya kanisa.

Hakika ndivyo ilivyokuwa. Namshukuru Mungu aliyenipa moyo wa kuyaandika niliyoyaandika. Kama unavyonifahamu 'kaka yako' kuwa mahali penye dhuluma huwa moyo wangu unaugua na kuhuzunika. Nimehuzunika hata kwa ajili yako.

Nijuavyo mpaka sasa ni kwamba wewe na Askofu Ambele Mwaipopo mlifukuzwa kutoka kikao cha Uteuzi cha Halmashauri Kuu na Mwenyekiti Askofu Dkt. Frederick Shoo.

Halmashauri Kuu ndio inayoteua majina ya wagombea wa nafasi ya Mkuu wa Kanisa. Ndipo majina hayo hupelekwa kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu kupigiwa kura.

Kufukuzwa kutoka Halmashauri Kuu maana yake ilikuwa ili majina yenu yasiwemo. Pamoja na maaskofu na wajumbe wa halmashauri kutaka muwepo ndani ya kikao, bado Mwenyekiti Shoo alikataa katakata na kusema 'hili ni lake na Bagonza'.

Labda Askofu Shoo hakuangalizwa vya kutosha juu ya jinsi alivyoonyesha chuki na visasi vya muda mrefu vilivyojaa wivu dhidi yako. Nakusihi wewe usamehe kwa ajili ya afya ya kanisa na huo ndio ushindi wako.

Kwa kifupi, pamoja na kutokuwepo kwako ndani ya kikao ili ujipigie kura, bado ulipigiwa kura nyingi vya kushangaza.

Kwa kuzingatia uhusiano wako na Mwenyekiti, ipo nafasi ya kuonea mashaka hata usahihi wa kura ulizopata kutoka kwa wajumbe. Kwanza hukuwemo ndani ya chumba kuhakiki hata mazingira.

Vilevile kwa namba zilivyoonekana, bila shaka kura yako ambayo ungejipigia ingekupasisha jina lako kwenda mbele. Siwezi kusema ikiwa ungepita, hivyo kama mwenyekiti angekubali kuwa jina lako lipelekwe Mkutano Mkuu.

Pia hatuwezi kusema matokeo yangekuwaje kama jina lako lingepelekwa Mkutano Mkuu kupigiwa kura.

Pamoja na hayo yote, wewe utabaki kuwa mshindi kwani hata hayo yaliyokukuta ni kwa sababu ya misimamo yako.

Mambo haya yote yawe ushahidi kwamba una nguvu na unaogopwa; na hivyo yakuimarishe katika imani na utume wako. Nikujuavyo huvumilii udhalimu kwa hiyo wadhalimu lazima wakuchukie.

Kwa hiyo, unachukiwa kwa mengi - unachukiwa kwa ubaya wako, unachukiwa kwa wema wako, unachukiwa kwa misimamo yako, unachukiwa kwa uchungaji wako na unachukiwa kwa uwezo wako wa kusamehe.

Nakusihi sana umsamehe sana Askofu Shoo kama nilivyomsamehe.

Tena nakusihi umsaidie Askofu Alex Malasusa aliyeangushiwa zigo la chuki, ufisadi, vinyongo, visasi katika kanisa ili Roho Mtakatifu ampe nguvu za kujenga kuta zilizobomoka.

• ***Mwandishi ni askofu (mstaafu) wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki. Ni mmoja wa wachangiaji wa Pambazuko.***

## Hoja Kinzani

# Posho kwa waandishi haramu, halali?

Na Tryruckia MFINANGA

KUMEKUWEPO mjadala wa muda mrefu – usiokufa, kuhusu uhalali au uharamu kwa waandishi wa habari kupokea posho wanapokuwa wakitekeleza majukumu na wajibu wao.

Mjadala huo haujawahi kupoa, kwa miaka nenda rudi.

Wapo wanaoeleza kuwa waandishi wa habari hawapaswi kupewa posho yoyote wanapokuwa wakifanya kazi zao, kwani kufanya hivyo, ni ngano ya kupoteza weledi wao, hasa wanapokuwa wakifanya kazi zenye maslahi mapana ya nchi.

Wengine wanadai kuwa posho kwa waandishi wa habari ni halali kwa kuwa tasnia yao haina tofauti na kada zingine wanapoalikwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao.

Kila kundi linajenga hoja zake na kuzitetea kwa maoni tofauti, lakini makundi yote yanabaki bila kupatikana kwa mshindi kwa maana hakuna jibu lenye kubeba dhima ya kuwafanya waandishi waonekane wao ni tofauti zaidi ya wengine.

Kimsingi, wanaoharamisha posho kwa waandishi wanadai ni sawa na rushwa, kiziba mdomo na majina mengine kuonesha siyo sawa kwa waandishi kupewa posho.

Wanaohalalisha nao wanadai posho kwa waandishi ni sahihi na haina maana ya takrima, kwani nao ni binadamu na wanapaswa kuwa na haki kama wengine.

Maswali kwa makundi haya yanabeba taswira ya watendaji wa kada nyingine, wakiwamo wabunge, majaji, mahakimu na wengine ambao, mara nyingi hualikwa kwenye semina, warsha, makongamano na mialiko mingine.

Posho wanazopewa watu kada hizi ni kuwezesha washiriki kupata fursa ya kujikimu; malazi, chakula, usafiri na shughuli zingine muhimu. Sasa je, mwandishi anapoalikwa, asipewe fursa ya kujikimu kwa sababu tu atashindwa kufanya kazi yake ya kuhoji na kuibua "madudu" kama yapo?

Ni kutokana na hofu ya waandishi kufungwa mikono na kuzibwa midomo na waalika, ndiyo maana kuliwahi kuibuka kampuni mbili za habari kuzuia waandishi wao kupokea posho, lakini hakuna mahali popote kwamba historia hiyo iliwahi kufanikiwa.

Kampuni za IPP Media na Mwananchi Communications, waliungana kutoa taarifa ya kukataa posho (bahasha) kwa waandishi wake, lakini hatua hii haikuwahi kuzaa matunda.

Kwanini? Kwa sababu haina uhalisia hata kidogo. Waandishi wake waliendelea kupokea posho, ingawa kwa kificho na msimamo huo ulikufa haraka mno, huku wamiliki wake wakikaa kimya hadi leo. Waligundua kukwama!

Ieleweke kwamba posho hutolewa kwa washiriki wa kusanyiko kwa maana ya kuwapa nafasi ya utulivu wa mawazo wanapokuwa wakishiriki semina na kuwapunguzia "mhemuko" wa mawazo kuhusu kula, kulala na hata kusafiri kurejea walikotoka.

Mwandishi makini, kama ilivyo kwa baadhi ya wabunge, majaji, askari, mahakimu na wanasheria, anaweza kufanya kazi yake kwa weledi mkubwa, akauliza maswali, akachambua hoja, akaibua madudu na kuyachapisha ama kutangaza, hata kama amepokea posho.

**Mwandishi ni mnufaika wa posho anapoalikwa, na hajawahi kuzibwa mdomo.**

# Polisi na tuhuma za uhaini kwa

**Na Joseph TADAYO**

WATU watatu walioelezwa kukabiliana na tuhuma za uhaini, waliachiwa huru kwa dhamana ya Jeshi la Polisi, hatua ambayo imeibua "sintofahamu" miongoni mwa jamii.

Kwamba iweje watu wanaotuhumiwa kupanga na kuhimiza kufanyika kwa uhaini wapewe dhamana, wakati kosa hilo halina nafuu hiyo kisheria?

IIjumaa iliyopita, Balozi Dkt. Wilbroad Slaa, wakili Boniface Mwabukusi na mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mpaluka Nyagali, almaarufu Mdude waliachiwa kwa dhamana ya Polisi.

Lipo swali linaloambatana unyanyapaa kwenye mitandao kwamba Imekuwaje wapewe dhamana wakati kosa la Uuhaini halina dhamana?

Nimejaribu kufuatilia kwa makini tangu sakata hili lilipoanza mpaka wakati Watanzania hawa wanaachiliwa kwa dhamana kuona ni lini au wapi walishtakiwa kwa kosa la uhaini, sijaweza kuona.

Baada ya Mahakama Kuu kutoa uamuzi juu ya kesi iliyoitwa ya "Mkataba wa Bandari," watu hawa wanaotuhumiwa kutoa matamko mbalimbali kwa nyakati na sehemu tofauti ambayo kwa tafsiri ya kawaida kabisa yanatengeneza kosa la uhaini chini ya kifungu cha 39(2)(d) cha Kanuni ya Adhabu( Penal Code).

Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania (IGP), Camillius Wambura akatoa onyo kali kwamba kuna watu wanatoa matamko ambayo yanayoashiria kusudio la kutenda kosa la uhaini dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. IGP wakati huo hakutaja jina la mmtu yeyote.

Ieleweke kuwa Mamlaka Polisi pale ambapo limetendeka jambo linaloashiria kosa lolote la jinai, ni kuchunguza na kujiridhisha kwamba hayo yaliyotendeka yanatengeneza kosa gani, chini ya sheria ipi.



*Balozi Dkt. Wilbroad Slaa*

Kumkamata mtuhumiwa, kumhoji na kuchukua maelezo yake ni sehemu ya uchunguzi, na sheria imeweka utaratibu kwa ajili ya kazi hiyo.

Kwa hiyo, Dkt. Slaa na wenzake walikamatwa kama sehemu ya uchunguzi, wakahojiwa, wakatoa maelezo hata kama siyo ya maandishi, na baadaye Polisi ikaridhika kwamba vitendo vyao vinatengeneza kosa ambalo lina dhamana kwa hiyo wakapewa dhamana.

Maneno yanaweza kuwa mengi kwamba wameshtakiwa kwa kosa la uhaini, lakini ukweli ni kwamba shitaka hutengenezwa na ushahidi ambao hupatikana kwenye upelelezi.

Kwa hiyo kabla Polisi hawajamaliza upelelezi, wasingeweza kusema watuhumiwa wanashtakiwa kwa kosa la uhaini.

Polisi wanayo haki na mamlaka ya kumtuhumu mtu kwa kosa kubwa na baada ya upelelezi wakaona kosa halisi ni dogo, na hivyo kufungua shitaka dogo, na pia wanaweza kutuhumu kosa dogo, lakini upelelezi ukabaini kosa kubwa.

Kwa hiyo, hakuna sababu za msingi za kulalamika au kukejeli kazi za Polisi kwa sababu mazingira ya kosa la jinai yalikuwepo, lakini upelelezi wa awali umebaini kosa lenye kupewa dhamana, hivyo hakuna jambo la ajabu.

**Mwandishi wa uchambuzi huu ni Mbunge wa Mwanga.**

# Tangazo


Ukiwa Bukoba...
Furahia
Nono
freshi Juisi
Pata juisi (sharubati) ya matunda halisi iliyoandaliwa kwa usafi wa hali ya juu kwa kujali afya ya mteja.
Kunywa juisi ya;
Maembe, Mananasi/pinacolada
Passion, Tende
Maparachichi,Matikiti, Karoti
Pia tunandaa juisi mchanganyiko maalum wa matunda ili kuondoa uchovu na magonjwa nyemelezi (detox) na pia smoothie.
Wasiliana nasi kwa namba hii:
0753949488
Nono
freshi Juisi
Pina colada

# Brics sasa yatamani Tanzania

**Na Mwandishi WETU**

KUENDELEA kuimarika kwa uchumi, uongozi bora, amani, kuzungukwa na nchi nane, kuwa pembeni mwa bahari, ni miongoni mwa sifa ambazo kundi la nchi zenye uchumi unaokua haraka (Brics) zinatamani Tanzania kuwa mwanachama wake mpya.

Kundi hilo lenye nchi tano hadi sasa, Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini (Brics), linaona pia uwepo wa bandari, mtandao mzuri wa barabara na malighafi nyingi, kuwa miongoni mwa vigezo vya kuijumuisha Tanzania kuwa mwanachama wake.

Pambazuko limedokezwa kwamba Tanzania ni nchi iliyojadiliwa zaidi na viongozi wakuu na wataalamu wa uchumi wa nchi za Brics waliokutana kwa ajili ya mkutano wao wa 15 katika Jiji la Johannesburg, Afrika Kusini kuanzia Agosti 22-24, mwaka huu.

Brics, kundi la kiuchumi lililoanzishwa rasmi mwaka 2006, likijumuisha nchi zenye uchumi unaokua haraka, limekuwa likielezwa na wachumi kwamba baada ya miaka 30 ijayo, litaongoza kwa kuwa na uimara wa uchumi duniani.

Tayari Brics imeanza kuhofiwa na Marekani, Umoja wa Ulaya (EU), Benki ya Dunia, na Shirika la Fedha ya Kimataifa (IMF), makundi ambayo Brics inatamani "kuyafuta" kwa imani kwamba yapo kwa ajili ya kunyonya zaidi kuliko kusaidia nchi zenye uchumi wa kati na masikini.

Pambazuko limeelezwa kwamba viongozi wakuu wa Brics, walipata wasaa wa kukutana na Rais Samia Suluhu Hassan na kwamba katika vikao vyao, wote walipongeza namna anavyoongoza nchi na kueleza matamanio yao "kuivuta" Tanzania kuwa mwanachama mpya wa Brics katika siku za usoni.

Hadi sasa Brics ina mwanachama mmoja kutoka Afrika, Afrika Kusini, nchi ambayo ilipewa uanachama mwaka 2010.

Katika mkutano wake uliomalizika huko Johannesburg wiki iliyopita, wakuu wa Brics waliongeza wanachama wengine wawili kutoka Afrika; Ethiopia na Misri, ambapo nchi hizo zitatambulika rasmi ndani ya kundi hilo kuanzia Januari, 2024.

Nchi nyingine zenye uchumi unaokua haraka; Argentina, Saudi Arabia, Imarati (UAE) na Iran nazo zitapata uanachama mwaka kesho, hivyo kufanya kundi hilo kuwa na wanachama 11.

Kuingizwa wanachama hao wapya kumezingatia vigezo ambavyo vingi Tanzania inavyo; mazingira mazuri ya uwekezaji, malighafi, madini, idadi kubwa ya watu na kuwa katika maeneo yenye jiografia-mkakati.

Kwamba jiografia ya Ethiopia, kwa maana ya kuzungukwa na rasilimali maji, bandari, uchumi unaokua na utulivu, pia kuwa na idadi kubwa ya watu ni vigezo vilivyoifanya nchi hiyo kuwa mwanachama wa Brics. Ethiopia ina idadi ya watu wanaofikia milioni 123.

Inaelezwa pia kwamba kuingizwa kwa Misri katika umoja huo kumetokana na kuwa na eneo la jiografia-mkakati, sambamba na kuwa na idadi kubwa ya watu. Nchi hiyo ina watu wanaokadiriwa kufikia milioni 112.

Akizungumza na Pambazuko kuhusu matamanio ya Brics kuwa na Tanzania, mtaalamu wa uchumi wa kimataifa, Dkt. Juma Khamis Ng'humayo anasema kuwa endapo Tanzania itakuwa mwanachama wa kundi hilo, uhakika wa uchumi wake kukua kwa haraka upo.

Anasema Kundi la Brics, katika miaka tisa iliyopita, lilianza kuitisha Benki ya Dunia na hata IMF kwa ya kuanzisha benki yake ya maendeleo na kuwekeza mtaji wa Dola za Marekani bilioni 250, ili kukopesha wanachama wake kwa riba na masharti nafuu.

Dkt. Ng'humayo ambaye ni mshauri wa uchumi, akifanya shughuli binafsi za ushauri anasema Brics kwa kuingiza wanachama wapya sita, itakuwa na nchi 11, ambazo uchumi wake – kwa maana ya

*Inaaendelea Uk. 9*

Habari

# Brics sasa yatamani Tanzania

*Inatoka Uk. 9*

pato la jumla, litakuwa ni theluthi moja ya uchumi wa dunia nzima.

Nchi hizo zitakuwa na mapato yanayofikia Dola za Marekani trilioni 34.

Naye Simon Mashauri, mtaalamu wa siasa uchumi anaeleza kwamba nchi wanachama wa Brics, huenda wakaitisha zaidi Marekani na mashirika ya fedha ya kimataifa kwa kuwa litakuwa kundi lenye nguvu kubwa ya kiuchumi lisilotegemea mashirika hayo; Benki ya Dunia, IMF na Markani kwa misaada na hata mikopo.

Anasema kuwa nchi hizo 11, ifikapo mwaka kesho, 2024, ndiyo zitakuwa wazalishaji wakubwa wa mafuta duniani kwa kuwa na asilimia 43 ya wazalishaji wote.

Miongoni mwa manufaa ya kuwa mwanachama wa Brics, ni kupata nafuu ya riba katika mikopo, kufanya biashara baina ya nchi wanachama kwa mazingira rafiki ya kodi na zaidi sana mwingiliano wa kubadilishana ujuzi katika maeneo ya sayansi, uchumi na nishati.

Brics pia imepanga kuanza kutumia sarafu zake ambazo zitaua matumizi ya kutegemea Dola ya Marekani au Pauni ya Uingereza na Euro ya Umoja wa Ulaya katika kufanya biashara.

Akizungumza baada ya Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa kutangaza nchi sita kuwa wanachama wapya wa Brics, Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed Ali aliandika katika ukurasa wake wa X (zamani Twitter) kuwa Ethiopia iko tayari kushirikiana na kufanya kazi ya kuleta maenedelo ya haraka.

Rais Mohammed bin Zayed Al Nahyan wa Falme za Kiarabu alisema; “tunaheshimu uamuzi wa uongozi wa BRICS ya kuamua kujumuishwa kwa

*Inaaendelea Uk. 11*




***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na Rais wa China, Xi Jinping kando ya Mkutano wa Brics uliokuwa ukifanyika katika Jiji la Johannesburg, Afrika Kusini – Hii ilikuwa Agosti 24, 2023. (Picha na Ikulu)***

# Brics sasa yatamani Tanzania

UAE kama mwanachama wa kikundi hiki muhimu."

Iran, ambayo ilitaja kujumuishwa kwake katika kundi hilo kama "ushindi wa kimkakati" kwa sera yake ya nje baada ya kukabiliwa na vikwazo vya nchi za magharibi na taasisi za fedha za kimataifa kwa miaka mingi.

**Mwanzo wa Brics**

Brics ni kifupi kilichotokana na "Bric", iliyobuniwa mwaka wa 2001 na mwanauchumi wa Taasisi ya Goldman Sachs, Jim O'Neil, kuashiria nchi nne zinazoendelea zenye uwezo mkubwa wa ukuaji - Brazil, Urusi, India na China.

Ongezeko la Afrika Kusini mwaka 2010, ambalo lilileta "S" kwa "Bric", kulifanya kundi hilo kuwa na takribani asilimia 40 ya watu wote duniani na karibu asilimia 25 ya uchumi wa dunia. Sasa takwimu hizi zitaongezeka kwa kuwepo wanachama wapya sita.

Mwaka 2006, mawaziri wa mambo ya nje wa nchi nne za kwanza katika kundi hilo walianza mkutano usio rasmi ambao ulisababisha mkutano rasmi wa mwaka 2009 kabla ya Afrika Kusini kuruhusiwa kuingia mwaka uliofuata.

Katika mkutano wa marais wa mwaka huu, viongozi wote wa nchi za Brics walikuwa Afrika Kusini, isipokuwa Rais Vladimir Putin wa Russia, ambaye alijiunga na mkutano huo kupitia mtandao, lakini aliwakilishwa na waziri wake wa mambo ya nje, Sergei Lavrov.

"India daima imekuwa ikiamini kwamba kuongezwa kwa wanachama wapya kutaimarisha zaidi kundi hili kama umoja wenye malengo ya wazi na yasiyokuwa na kificho," alisema Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi.

Rais Xi Jinping wa China alielezea kufurahishwa kwake na kuongezeka kwa wanachama wa kundi hilo kuwa ni hatua ya "kihistoria" inayoonesha dhamira ya nchi husika kuwa na uchumi imara.

Katika hotuba iliyorekodiwa kwenye mkutano wa Brics, Rais wa Urusi, Vladimir Putin alisema kundi hilo liko mbioni kukidhi matarajio ya idadi kubwa ya watu duniani.

"Tunashirikiana kwa kufuata misingi na kanuni za usawa, kuheshimu maslahi ya kila mmoja wetu, na hii ndiyo kiini cha mwendo wa kimkakati wenye mwelekeo wa siku za usoni wa Brics," aliongeza Putin.

**Mipango ya muda mrefu**

Wachambuzi wanaamini kuwa muungano huo wa kiuchumi ulioongezwa nguvu unaweza kubadilisha jinsi mambo yanavyofanya kazi katika ufadhili wa kimataifa.

"Muungano huu wa kimataifa sasa utakuwa chombo chenye nguvu na kiwango kikubwa zaidi cha pato la taifa," Dkt. Isa Abdullahi wa Idara ya Uchumi katika Chuo Kikuu cha Kashere, Nigeria aliiambia TRT Afrika.

"Inachoonesha ni kwamba tutakuwa na mwelekeo mpya wa kimataifa, na utaratibu mbadala wa kifedha wa kimataifa."

Kwa upande mwingine, matarajio ya Brics yanakabiliwa na changamoto kubwa kutoka kwa wale wanaosimamia fedha za kimataifa kwa sasa.

"Hata hivyo, haitakuwa rahisi kwa Brics kujiendeleza kwa njia hii, bila shaka, bila kuwa na changamoto kutoka kwa mashirika ya jadi kama vile IMF, Benki ya Dunia, Klabu ya Paris, Klabu ya London na kadhalika," Dkt. Abdullahi alisema.


"Habari njema ni nguvu ya pamoja ya kifedha ya shirikisho lililopanuliwa la nchi zinazoendelea kiuchumi. Pamoja na wanachama wapya kama Saudi Arabia huja na kiasi kikubwa cha fedha…

… Argentina pia, kikundi kitakusanya nguvu zaidi, watakusanya utajiri zaidi. Watakuwa na njia mbadala za kifedha badala ya mashirika ya jadi ya kimataifa yenye jukumu la ufadhili duniani kote," aliongeza Dkt. Abdullahi.

Sulaiman Dahiru, balozi wa zamani wa Nigeria nchini Sudan, anaamini kuwa upanuzi wa Brics unalenga kutoa changamoto kwa utawala wa kiuchumi wa nchi za magharibi, hasa Marekani.

## Habari katika Picha

# Chadema 'yashambulia' Shinyanga














***Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, akiendelea na kampeni ya chama chake kuandikisha wanachama wapya na kuzungumza na Watanzania juu ya mustakabali wa nchi yao kwa jicho la chama hicho cha upinzani. Hapa ni picha mbalimbali zikionesha shughuli za kiongozi huyo mkoani Shinyanga juzi na jana. (Picha na Chadema).***


100% TRUSTED BRAND
PROUDLY TANZANIAN PRODUCT
DOR EASY WASH
LIQUID SOAPS
USAFI WAKO
NI JUKUMU LETU
MANUFACTURED BY: DOR EASY WASH
P.O BOX 80159 KIBADA, KIGAMBONI | DAR ES SALAAM - TANZANIA
MOB: +255 715 771 123 | EMAIL: DOREASYWASH@GMAIL.COM

Jamii

# Polisi wajikite kuzuia ukatili wa kingono

Na Protas KANEMELA

UKATILI wa kingono kwa watoto wadogo ni janga ambalo bado linasumbua jamii na kwamba bado kuna safari ndefu ya kulikomesha.

Watoto wengi wa kiume na wale wa kike, wamekuwa wakifanyiwa vitendo vingi vya ukatili wa kingono bila wao kutambua wamefanyiwa, ikiwa ni pamoja na kutomaswa, kuguswa sehemu za siri na wengine kuingiliwa na ndugu wa karibu.

Katika jamii yetu kumekuwa na matukio mengi ambayo watoto wengine wakiulizwa hutoa sababu za chanzo cha kuingizwa kwenye ukatili huo kuwa ni kuangalia picha cha utupu, picha za ngono na wengine kutumia simu kuangalia picha zinavyoashiria vitendo vya ngono.

Jamii, serikali, taasisi na mashirika ya watu binafsi wamekuwa wakipaza sauti kutokana na kutokea kwa vitendo vingi vinavyosababisha kuwepo kwa ukatili wa vitendo vya kingono kwenye jamii.

Kuna baadhi ya matukio yamekuwa yakitolewa taarifa ila kutokana na ukosefu wa ushahidi na walengwa kutojitokeza kwenye vyombo vya sheria, imekuwa ikisababisha kesi nyingi kutoendelea na kusababisha kufutwa kwa kukosa ushahidi.

Taarifa kutoka kwenye vyombo vya sheria zinaonyesha kuwa baadhi ya wazazi na walezi wameshindwa kuwajibika kwenye malezi ya watoto na wengine kutokuwa karibu nao, kumesababisha kuongezeka kwa vitendo hivyo vya ukatili wa kingono kutoka kwa ndugu wa karibu ndani ya familia.

Ofisa Polisi Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Iringa, Elizabeth Swai anasema baadhi ya wazazi wanaona kuwa suala la malezi ni kutoa mahitaji ya msingi kwa mtoto kama kumpeleka shule na kusahau kuwa kutofuatilia maendeleo yao kunaweza kuchangia ongezeke la ukatili wa kingono.

Swai anaongeza kuwa baadhi ya



*Mkuu wa Jeshi la Polisi Camillius Wambura*

matukio ya ukatili hayafikishwi katika vyombo husika kutokana na wazazi kusuluhisha katika ngazi ya familia, jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Anaongeza kuwa ndugu wa karibu wamehusika katika kuficha ukweli na matukio yapo.

Anasema kwa sasa Jeshi la Polisi linafanya kazi ya kupita shuleni na kuwaelimisha watoto na wamekuwa wakitoa taarifa kwenye vituo vya Polisi na kufungua kesi jambo linaloweza kupunguza vitendo vya ukatili wa kingono.

Ukiangalia matukio kama hayo mengi kwa mujibu wa sheria, yana muda wa kufikisha kwenye vyombo vya kikanuni ambapo Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaaa ya Iringa, Leah Frank anasema kwa muda wa saa 72 ikitolewa taarifa husaidia kupata haki kwa mtoto.

Leah anaongeza kuwa kuchelewa kutoa taarifa za vitendo vya ukatili chini ya saa 72 kunapoteza ushahidi na kumkosesha mtoto haki yake ya kimsingi na wengine kusababishwa kuambukizwa magonjwa ya zinaa ikiwemo maambukizi ya Ukimwi.

Leah anashauri kwamba ni vyema Polisi kuimarisha mafunzo kwa wanafunzi ili watambue namna ya kuripoti matukio ya ukatili hasa ya kingono.

## Tangazo


# Tangaza na Pambazuko

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.




## Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au Barua-Pepe; **info@pambazuko.tz**

## Maono

# Tunza afya, ni utajiri usiofananishwa

Na Mwandishi MAALUM

SEPTEMBA 9 – siku 13 kutoka leo, dunia ya wapenda mitindo, muziki na wapenzi wa mashahiri, wataungana na kuadhimisha miaka sita tangu kufariki kwa mwanamitindo, Crisda Rodríguez.

Crisda, mwanadada aliyefariki dunia akiwa na miaka 40; mwaka 2018, baada ya kuugua saratani ya utumbo mpana, atakumbukwa na namna alivyojitolea kusaidia vipaji vya sanaa kwa vijana wa New Jersey, Marekani na nchi alikozaliwa, Jamhuri ya Dominika.

Pia tasnia ya habari itamkumbuka kwa namna alivyopata umaarufu mkubwa baada ya kujiunga na vituo kadhaa vya televisheni akiwa mwandishi na mtangazaji.

Mbali na sifa hizo za Crisda, jambo kubwa zaidi analoendelea kukumbukwa nalo hadi sasa ni namna alivyoandika waraka, muda mfupi kabla ya kufariki kwake dunia ambao unabeba ujumbe mzito unaoendelea kuwa rejea hadi leo.

Kabla ya kufariki dunia Crisda Rodríguez aliandika maneno haya akiwa kitandani na kuyahifadhi kwenye shajara (diary) yake ndogo:

Nilikuwa na gari la gharama kubwa zaidi duniani katika karakana yangu, lakini sasa inabidi nitumie kiti cha magurudumu kujisogeza.

Nyumba yangu ilijaa kila aina ya nguo zenye chapa (designers), viatu, na vitu vya thamani, lakini sasa mwili wangu umefungwa kwa kitambaa kidogo nilichopewa na hospitali.

Nina pesa nyingi benki. Lakini sasa sinufaiki na kiasi hicho kikubwa.

Nyumba yangu ilikuwa kama ngome, lakini sasa ninalala katika kitanda hospitalini.

Kutoka hoteli ya nyota tano hadi hoteli ya almasi, lakini sasa hivi mimi hutumia muda katika hospitali kuhama kutoka maabara moja hadi nyingine.

Nilikuwa na vinyozi saba wa kurekebisha nywele zangu, lakini sasa, sina hata unywele mmoja kichwani mwangu.



*Crisda Rodríguez*

Kwenye ndege ya binafsi, niliweza kuruka popote, lakini sasa ninahitaji usaidizi wa watu wawili ili kutembea hadi lango la hospitali.

Ingawa kuna vyakula vingi, sasa mlo wangu ni vidonge viwili kwa siku na matone machache ya maji ya chumvi usiku.

Hii nyumba, gari hili, ndege hii, samani hizi, benki hii, sifa na umaarufu kupita kiasi, hakuna hata kimoja chenye manufaa kwangu. Hakuna kati ya haya kitakachonipumzisha.

“Hakuna kitu halisi isipokuwa kifo.”

Mwisho wa siku, utajiri mkubwa zaidi kwenye maisha ya binadamu ni afya njema yake.

Kama umejaaliwa kuwa na afya njema japo kwa kiasi kidogo, furahia maisha yako kwa hata kwa chochote kidogo ulichonacho.

Kuna watu wanatamani kuinunua afya yako kwa gharama yeyote ile kama ingewezekana, lakini huenda hilo lisowezekane kwa kuwa nawe bado unahitaji utajiri huo wa afya.

Wewe mwenye afya ni tajiri mkubwa, jipige kifua kufurahi na kumshukuru Mungu na zaidi sana acha kiburi na pata muda wa kusaidia wengine.

# Kijana jiamini, maisha yapo mtaani

**Na Martha NGHAMBI**

TAASISI za elimu kuanzia darasa la saba, kidato cha nne, kidato cha sita, vyuo mbalimbali vya ufundi na vyuo vikuu, vinazalisha idadi ya wahitimu kila msimu.

Takwimu za Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) zinaonesha ongezeko la udahili wa wanafunzi wa ngazi ya cheti mpaka uzamivu (PhD) wa taasisi za elimu ya juu kufikia 213,829 (2017/17) mpaka kufika 314,643 (2022/23).

Hii inatupa picha ya idadi kubwa ya wanafunzi wanaomaliza licha ya kwamba wachache wao wanakatiza masomo.

Wahitimu hao wanaondoka wakiwa na matumaini ya maisha bora kwa kupata ajira zenye tija.

Lakini hali halisi ikoje? Pengine, wote tukawa na jibu kwa sababu sisi ni sehemu ya jamii ambayo vijana hawa wapo. Huenda katika familia zetu ama jamii zetu tumeshuhudia vijana hawa wakihangaika kupata walau kibarua cha kujiingizi kipato.

Siyo ajabu hata kukutana na wahitimu wa vidato na shahada mbalimbali wakiwa katika hekaheka hizi za kusaka ajira mitaani.

Kwa kipindi kati ya mwaka 2015 hadi sasa kumekuwa na wimbi kubwa la vijana wa namna hii. Na mara nyingi Vijana wengi ni wale wanaotoka katika kaya masikini, ambapo mpaka anamaliza masomo, kuna gharama kubwa imelipwa na familia.

Kutokana na hili, kijana anajikuta ana mzigo mkubwa wa matazamio ya wazazi, ndugu na jamaa nyuma yake. Hili huongeza sonona kwa kijana.

Hivyo basi, athari zake ni vijana kujikuta wanajiingiza kwenye vitendo vibaya ili mradi tu maisha yaende wakati akipambana.

Lakini wapo wachache wanaoamua kuweka elimu zao pembeni na kufanya kazi ambazo zinaonekana hazina staha.

Niliwahi kumuona binti mmoja, mhitimu mmoja wa chuo kikuu akiuza mahindi ya kuchoma barabarani. Hili ni jambo la huzuni, ingawa anaweza kujiongeza kwa kuongeza thamani ya biashara yake hiyo.

Lakini, suluhisho la kudumu ni nini? Pengine tunaweza kujifunza kwa ushauri alitoa hivi karibuni, Christopher Ngubi, Mkuu wa Wilaya Kilwa ambapo aliwasihi

*Endelea Uk. 18*



*Ajira ni ajira, moradi kupata kipato. Vijana wasichague kazi*

Makala

# Kijana jiamini, maisha yapo mtaani

*Inatoka Uk. 17*

vijana kuwa wasione aibu kuweka usomi pembeni na kutafuta njia mbadala ya maisha.

Kiongozi huyo aligusia kuwa maarifa peke yake hayatoshi hasa katika mazingira yetu, bali ujuzi.

Hii maana yake ni kwamba kijana badala ya kukumbatia cheti cha shahada, anaweza kujifunza stadi maalum ambazo zinahitajika mtaani kwa sasa kama ufundi magari, mapishi, ubunifu mashine, kilimo cha kisasa, uvuvi n.k.

Aidha, Ngubi alitoa rai kwa taasisi zetu za elimu kubadilisha mfumo wa elimu ili kwenda na wakati na changamoto za sasa za maisha na uelewa.

"Badala ya kutoa shahada zilizopitwa na wakati, tukazanie zaidi elimu ya ufundi. China na nchi kadhaa zinazoendelea zimetoa mfano bora wa njia ya kusaidia makundi ya vijana" anaongeza mkuu huyo wa wilaya.

Akizungumzia mikakati ya Wilaya ya Kilwa kusaidia vijana, hasa wahitimu wa vyuo kujitegemea, Ngubi, amesema kutaanzishwa kituo Maalum cha Vijana (ICT Center) ambacho kitahusika na kuratibu mipango ya kusaidia vijana.

Amebainisha kuwa kituo hicho kitaanzishwa kwa ushirikiano na Shirika la Global Peace Foundation na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Vijana wataweza kupata taarifa za fursa mbalimbali za biashara, ajira, masomo na mikopo na mengine mengi kupitia kituo hicho.

Aidha, kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Filberto Sanga alitanabaisha kwamba kundi la vijana lina changamoto nyingi. Kundi hili linahangaika kujiandaa na maisha ya sasa na baadae.

"Kila kijana anatamani kupata maendeleo kwa kasi, wakati huo anashindana na wenzake bila kujali wenzake wanatumia mbinu gani kupata mafanikio. Na yeye anajikuta anatumia njia ambazo hazitakiwi ili afanikiwe haraka. Hata akiambiwa 'pale kuna madawa ya kulevya, kasafirishe kule utapata utajiri, yuko tayari," ameongeza.

Sanga anasema kuwa vijana wengi kwa sasa wako tayri hata kushiriki kuiba na shughuli zingine haramu ili tu aweze kupata fedha, bila kuangalia madhara yake.

Anasema maeneo mengi duniani, takwimu zinaonesha kuwa vijana ndiyo kundi linaloongoza kwa kuwa na matukio ya uhalifu, kiasi kwamba hata magereza mengi yamejaa vijana ambao wangeweza kutumia ujuzi wao kupata kipato halali.

"Hata kwenye uvunjifu wa amani katika mataifa mbalimbali, sehemu kubwa wanaotumika ni makundi ya vijana. Hata hapa kwetu, wahalifu hulenga kutumia vijana kufanikisha malengo yao maovu,"amesema mkuu huyo wa wilaya.

Mratibu wa Masuala ya Vijana katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Dkt. Nassibu Richard Mwaifunga - kwa upande wake alisema serikali ina utaratibu wa kusaidia vijana kujiinua kiuchumi kupitia nafasi za mikopo ya mtu mmoja mmoja, masomo ndani na nje ya nchi na fursa za kusaidia vijana waliomaliza masomo kupata ujuzi kivitendo.

Mmoja wa vijana walioshiriki semina hiyo, amesema; "kama umekosa ajira usikae tu, inabidi vijana tujiongeze kwa kuangalia fursa ambazo zipo Ili kuweza kuwa na amani lazima tufanye kazi kwa bidii kujitafutia riziki."

Kijana huyo, Jane Songalele kutoka Nyasa, anasema watu wasiogope kuchukua mikopo bali waione kuwa ni fursa na wakiipata wahakikishe wanarejesha kwa wakati ili kuendelea kuaminika.

**** Makala haya yametokana na zoezi la uandaaji Mradi wa Dumisha Amani kwa Maendeleo Endelevu unaosimamiwa na Shirika la Global Peace Foudation Tanzania kwa ushirikano na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Ofisi ya Waziri Mkuu unakelezwa katika Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara.***

# Yanga kuivaa El Merreikh Rwanda




**Na Mwandishi WETU**

MABINGWA wa Tanzania, timu ya Yanga itavaana na El Merreikh ya Sudan katika hatua ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kipute hichi kitapigwa katika Uwanja wa Huye ulioko nje ya Jiji la Kigali. Uwanja huo unaotumiwa na Timu ya Mukura Victory Sports, umechaguliwa na timu hiyo ya Sudan kuwa uwanja wake wa nyumbani.

Inatarajiwa kwamba timu hizo ziacheza kati ya Septemba 15-17, na kwamba mechi ya marudiano ikipangwa kati ya Septemba 29 hadi Oktoba Mosi.

Endapo Yanga itawafunga hao Wasudani, itakuwa imepata tiketi ya moja kwa moja hatua ya makundi itakayoanza kati ya Novemba 24-26.

Yanga, ambao pia ni washindi wa pili wa Kombe la Shirikisho – 2023, imetinga hatua hiyo baada ya kuichabanga Timu ya Asas ya Djibouti kwa jumla ya mabao 7-1.

Timu ya Asas, ambayo imechagua Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, ilifungwa mabao 2-1 na wiki iliyopita “kuvurugwa” kwa kupigwa mabao 5-1.

Katika mchezo wao wa marudiano, mabao ya wenyeji – Yanga, yalifungwa na Maxi Nzengeli aliyefunga mawili (dakika ya 7 na 90), Hafiz Konkoni (45), Pacome Zouzoua (55) na Clement Mzize (69).

Asas walipata bao la kufutia machozi kufuatia mkwaju wa uliowekwa kimiani na Tito Lukciir Madul Mayor katika dakika ya 85.

Katika mchezo wa kwanza, ambao Yanga iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 ambayo yalifungwa na Kennedy Musonda na Stephane Aziz KI.

Nayo El Merreikh inatinga hatua ya kupambana na Yanga baada ya kuifunga Timu ya AS Otoho d’oyo ya Congo (Brazzaville) kwa kupata faida ya bao la ugenini, baada ya timu hizo kufungana bao 1-1 katika mechi ya kwanza iliyochezwa wiki iliyopita kisha juzi - Jumamosi kutoka suluhu.

# NANI KAMA MAMA...



*Mama Maria Nyerere, mke wa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, akikumbatiwa na Graca Machel, mke wa aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Nelson Mandela. Graca alimtembelea Mama Maria nyumbani kwake Msasani, Dar es Salaam alipokuwa nchini Tanzania hivi karibuni – Julai, 2023. (Picha na Ikulu)*

*GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION